

Jina: .....

Nambari: .....

Shule: .....

Sahihi .....

Tarehe: .....

**102/3**

**KISWAHILI**

**FASIHI**

**KARATASI YA 3**

**MUDA: 2 ½**

# **MTIHANI WA MUUNGANO KANDA YA BUTERE MASHARIKI**

*Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya. (K.C.S.E)*

**KISWAHILI**

**FASIHI**

## **MAAGIZO**

- *Jibu maswali manne pekee*
- *Swali la kwanza ni lazima*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nnne zilizobaki yaani, riwaya , Ushairi hadithi fupi na fasihi simulizi.*
- *Usijubi maswali mawili kutoka sehemu moja.*

*Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**SEHEMU YA A : THAMTHILIA**  
***KIFO KISIMANI: Kithaka wa Mberia***

1. Fafanua jinsi ASkari wa mtemi Bokono pamoja na washauri wake wanavyoendeleza dhuluma nchini Butangi. (ala. 20)

**SEHEMU YA B: HADITHI FUPI**

***MAYAI WAZIRI WA MARADHI: K.W Wamitila.***

***Jibu swalî la 2 na 3***

2. Eleza dhana ya udunishaji wa mwanamke katika hadithi ya “Uteuzi wa moyoni n aNgome ya nafsi”.
3. “Alikiuma kidomo chake na kuchukua hatua ya mwisho. Moyoni alihisi ndimi za aina yake zikimwunguza. Ndimi za mauti.”
- a) Fafanua muktadha huu. (ala.4)
- b) Kwa kutolea mifano fafanua aina zozote mbili za ndimi kulingana na hadithi hii. (ala.4)
- c) Ni sababu gani zilizochngia mkasa huu kufikia kiwango ulichofikia (ala.4)
- d) Fafanua majuto kwa kila mtekezi wa mkasa huu. (ala 8)

**SEHEMU YA C :RIWAYA**

***S.A Mohamed : UTENGANO***

***Jibu swalî la 4 na 5***

4. Sikiliza, dunia hii hayendi bila ya pesa. Unapokuwa ukii...unapokuwa kiongozi piga kelele. Taja kila kitu lakini unapopata nafasi ya kula, kula
- a) Eleza muktadha wa dondo hili. (ala 4)
- b) Ni mbinu gani ya lugha imetawala kijfungu hiki cha maneno ? (ala.2)
- c) Eleza umuhimu wa mnenaji wa maneno haya katika riwaya hii, (ala.14)
- 5 . Huku ukitoa mifano mwafaka jadili maudhui ya kisasi katika riwaya ya utegnano. (ala. 20)

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

6. ***Soma shairi lifatalo kasha ujibu maswali yanyo fuatia.***

Unganiambia ni mui, kattu simwati wema,  
Wewe ndiye wangu kui, nalousiwa ni mama,  
Leo kwamba siujui, ni kupotosha heshima,  
Siasi kutenda wema, kaandama wadui.

Wema nambiwa na andia, hadi bandari salama,  
Hayo naliyosikia, nao wahenga wa zama,  
Peny wema tajitia, niipate kaadhima.  
Siasi kutenda wema, japo munganinunia.

Na iwe kupawa mali, ya kuhadaa mtima  
Niandame ufidhuli, nitengana nao wema  
Hilo sitokubali, japo waja wangsema,  
Siasi kwenda wema , ujapokuwa ni ghali

Sitomehe kabaila, nganitenza nache wema,  
Mungunitia na jela, kisa mefanza huruma,  
Haragwe lenu talila, pamoja na yenu sima,  
Siasi kutenda wema, japo tagoni talala

Haufi mungaufisha, auhamipo karima.  
Mola atauhusisha, welekeapo kuzama  
Mimi ni huo maisha, hadi siku ya kiama  
Siasi kutenda wema, nganitia mshawasha.

Wema ungawa mchungu, tajaribu kutotema,  
Tautenda nende zangu, niache wanaosema,  
Malipo yangu kwa mungu, hayo yenu si lazima  
Siasi kutende wema, kiaghari mu ro ho yangu.

### Maswali

- a) Ni mambo yapi katika ubeti wa 1 hadi 4 ambayo hata mshairi akifanyiwa hawezi kuacha kutenda mema? (ala.6)
- b) Eleza jinsi mtunzi wa shairi hili alivyoutumia uhuru wake. (ala.6)
- c) Andika ubeti wa mwisho katika lugha nathari. (ala.4)
- d) Mshairi alipata wapi ari ya kuzingatia wema? (ala.2)
- e) Mshairi ana imani gani kwa Mungu? (ala.2)

### **SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

- 4. a) Maghani ni nini? (ala. 2)
- b) Eleza fani zifuatazo za magahni. (ala 8)
  - i) vivugo.
  - ii) Tondozi.
  - iii) Pembezi.
  - iv) Rara
- c) Eleza maana ya neno ulumbi. (ala 2)
- d) Bainisha sifa za mlumi (ala 8)